THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS BOARD

# DARASA LA SITA - KNEB 2021

PRE - GOLD

## KISWAHILI: LUGHA

@ii@ii

*Muda: Saa I dakika 40*

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.*

Sisi __1__ na mama __2__ mkali sana. Mama __3__ hakuturuhusu __4__ sheria zozote kimboni petu. Kila alipohisi kuwa __5__ kuoga, alitulazimisha kuoga maji baridi lakini __6__ kutumia sabuni mbayo __7__ vizuri sana. Au kila alipogundua __8__ utovu kinidhamu, tulikaripiwa na kukumbushwa kuwa ulikuwa wajibu __9__ kuwalinda wavyele wetu kwa tabia.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. tulilelewa | B. tulielewa | C. tulilelea | D. tulilea |
| 2. | A. aliyokuwa | B. aliyekuwa | C. aliyekua | D. aliokuwa |
| 3. | A. huo | B. hio | C. huyo | D. hilo |
| 4. | A. kuvuja | B. kufunja | C. kufuja | D. kuvunja |
| 5. | A. tuliogopa | B. tumeogopa | C. tutaogopa | D. wanaogopa |
| 6. | A. ingawa | B. na | C. kwa | D. kuwa |
| 7. | A. ilinukwa | B. ilinukia | C. inanukia | D. ilinuka |
| 8. | A. tuna | B. mna | C. wana | D. lima |
| 9. | A. wangu | B. wetu | C. wao | D. yetu |

Mawasiliano ni kitendo cha __10__ ujumbe. Hii ni __11__ binadamu sanasana. Kuna njia __12__ za mawasiliano. Kunazo zile za jadi kama vile kuwasha moto, kupiga uyoma na utum watu maalum __13__ ujumbe mahali ulipohitajika, siku hizi, watu __14__ simu, magazeti, majanida na vifaa __15__ kuwasiliana.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 10. | A. kupishana | B. kupashia | C. kupashika | D. kupashana |
| 11. | A. licha ya | B. katikati ya | C. baina ya | D. mithili ya |
| 12. | A.' mingi | B. nyingi | C. jingi | D. mingi |
| 13. | A. kuupeleka | B. kuzipeleka | C. kulipeleka | D. kukupcleka |
| 14. | A. walitumia | B. hutumia | C. wametumia | D. wangetumia |
| 15. | A. nyinginezo | B. zinginezo | C. mengineyo | D. vinginevyo |

Ecolebooks.com

O Stepford Press and Publishers. 2021

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Kuanzia swali la 16-30, jibu kila swali kulingana na maagizo.

**16.** Chagua orodha ambayo ni ya vielezi

A. hivi, nyingi, yoyote, chake
B. nyinyi, wewe, mimi, sisi
C. sana, upesi, hakika, kabisa
D. lini, gani, vipi, mbona

17. Chagua kiashiria takriri kilicho sahihi kujaza pengo:

Vikombe ______ vilianguka hapa.

A. vivi hivyo
B. hivyo hivi
C. hivi vivi
D. vivi hivi

18. Jaza pengo kwa neno sahihi:

Mama alienda shambani na alishinda kule huko mchana ______

A. kutua
B. kutwa
C. kutwaa
D. kucha

**19.** Ni yupi mpangilio uletao mfululizo ufaao wa wakati?

A. Alfajiri, asubuhi, adhuhuri, alasiri magharibi
B. Alasiri, asubuhi, alfajiri, magharibi adhuhuri
C. Asubuhi, alfajiri, alasiri, adhuhuri, magharibi.
D. Alfajiri, asubuhi, alasiri, adhuhuri, magharibi

20. Umbo hili ni

A. duara
B. mche
C. mpira
D. duara dufu

**21.** Mnyama ana manyoya mwilini, naye binadamu ana

A. nywele
B. malaika
C. ndewe
D. mashamba

A. kifo
B. kioo
C. kumetameta
D. kivuli

23. Kutangaza kwa sauti kubwa ni

A. kupiga maji
B. kupiga mayowe
C. kupiga mbiu
D. kipiga domo

24. Chagua kinyume cha sentensi ifuatayo:
Kitindamimba alifurahi sana.

A. Kifunguamimba alifurahi sana.
B. Kitindamimba alikasirika sana.
C. Mwanambee alifurahi sana.
D. Mwanambee alikasirika sana.

25. Kanusha: Nimekula nikashiba

A. Sijala nikashiba.
B. Sijakula nikashiba.
C. Sijala wala kushiba.
D. Sikula wala kushiba.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM


26. Jazapengokwausahihi:Nyinyi.mli ____ talikakaramuni.A.nd inyi/o
B. ndiwo/ wo
C. ndio/ o
D. ndio/ ye

27. Tunasema shungi la nywele ___ a kuni pia ___ la mchanga.
A. chanc/ tita
B. tita/ fungu
C. shado/ koja
D. kicha/ bumba

28. 3, 7, 17, 31 na 43 ni baadhi ya nambari
A. tasa
B. shufwa
C. chanya
D. witiri

29. Kamilisha sentensi kwa usahihi:
Mahali hapa palifye kwa
A. pakafyekana
B. pakafyekeshwa
C. pakafyekeka
D. pakafyekewa

22. Tegua kitendawili hiki:
Mava hapo mava pale



30. Katika milioni sita kuna laki ngapi?
A. Sita B. Sitini
C. Elf sita D. Mia sita

Ecolebooks.com



*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka* ***40.***

Mango ulibishwa. Bakari akachungulia kwenye tundu la mlangoni. Akaona mwanamke na mwanamume wamesimama wamebeba matunda. "Baba na mama wako?" waliuliza watu wale wawili. "La, hawapo, wameenda sokoni," Bakari alijibu.

"Basi watakapokuja wasalimie na uwape matunda haya na kuku huyu," wakamaliza. "Ngojeni niwapokee. msiende tafadhali." Bakari alisema huku akifungua mlango. Kufumba na kufumbua, Bakari alijikuta amewekewa bastola kichwani. "Funga mdomo wako ukitaka usalama wako, ng'ombe wewe. Nyinyi mnashiba na watu wafa njaa!" Alisema mwanamume yule kwa **ghadhabu.** "Pesa, dhahabu na vyombo vya mama yako viko wapi?" Mwanamke aliuliza huku akizaba Bakari makofi mawili mazito. Bakari akamwonyesha kila kitu kwani roho yake ilikuwa mikononi, alikuwa hajijui hajitambui!

Wezi wale wawili wakaisafisha nyumba na kuifanya msikiti. Wakampulizia Bakari dawa ya usingizi. Papo hapo akaanguka na kulala fofofo!

**31.** Bakari alikuwa na nani nyumbani?

A. Pekee
B. Bibiye
C. Rafiki yake
D. Mama na baba

32. Watu wale wawili waliuliza akina nani?

A. Baba
B. Wazee
C. Baba na mama
D. Mama

33. Ninini kilichomfanya Bakari afungue mlango?

A. Alishurutishwa kufanya hivyo.
B. Zawadi alizoambiwa ni za wazazi wake.
C. Alitaka kuwaona wageni wale vizuri.
D. Aliwaona mwanamume na mwanamke.

**34.** Bakari alipigwa makofi na nani?

A. Mamake
B. Rafikiye
C. Mwanamume yule
D. Mwanamke yule

35. 'Kufumba na kufumbua' ina maana gani?

A. Hapo hapo
B. Mara kwa mara
C. Baadaye
D. Kwa haraka kabisa

36. Kumpokea mtu ni kufanya nini?

A. Kumchukia
B. Kumkaribisha
C. Kumwongelesha
D. Kumfungulia mlango

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

37. Kuwa roho mkononi ni sawa na kusema
   A. kuwa karibu kufa.
   B. kuwa na woga zaidi.
   C. kwenda na roho kwenye mkono.
   D. kubeba roho kwenye mkono.

38. Wezi walilalamikia nini?
   A. Kutofunguliwa mlango.
   B. Wao kushiba na watu kufa kwa njaa.
   C. Kutokweko na wazazi.
   D. Kutopata dhahabu, vy'ombo na pesa.

39. Wezi hawa wangeshikwa wakijba ungewaambia methali gani?
   A. Siku za mwizi ni arubaini.
   B. Mtaka yote hukosa yote.
   C. Bendera hufuata upepo.
   D. Mtegemea cha nduguye hufa masikini.

**40.** Neno **ghadhabu** lina maana gani kuligana na ufahamu?
   A. Elekeza
   B. Haraka kabisa
   C. Hofu kubwa
   D. Kukasirika

*Soma kifungukifatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.*

Simu ni chombo cha watu cha kuwasiliana. Simu hutumia mawimbi ili kupokea sauti au picha. Kuna aina mbiliza simu. Rununu na simu ya ofisi.

O *Stepford Press and Publishers, 2021*

Ecolebooks.com



Simu ya ofisi au simu ya nyumbani mara nyingi hutumiwa ofisini ama nyumbani. Simu hii huwekwa mahali fulani maalum katika ofisi. Simu hii huwekwa katika mapokezi. Inapopigwa, huwezi kuona nambari ya anayepiga.

Rununu pia huitwa simu tamba, selula au rokono. Rununu ni simu ndogo ambayo unaweza kuibeba mahali popote unapoenda. Rununu hutumia simu kadi. Pia hutumia kadihela ili kupata muda wa maongezi. Manufaa ya rununu ni **tumbi tumbi**. Hata kama ni ndogo wahenga walisema usione wembamba wa reli, gari moshi hupita.

Manufaa ya rununu ni kuwa huweza kutuma arafa. Arafa ni ujumbe mfupi unaotumwa kwa njia ya kuandika. Pia, hutumika katika biashara kwa kutuma pesa za kununua bidhaa.

Simu pia hutumika kuwapa watu ajira kwa kuajiriwa katika duka la M-pesa, kuuza rununu na vifaa vyake. Watu wengine huzitengeneza simu zilizoharibika kwa malipo na wao hupata ajira.

Hakuna kizuri kisichokuwa na hila. Rununu ina hasara pia. Inaweza kutumiwa na waovu kuwaibia watu pesa. Aidha kutuma ujumbe wa chuki, matusi na picha chafu zisizofaa.

Daima, tutumie rununu kwa uangalifu mkubwa tusije tukajuta majuto ya mjukuu ambayo huja baadaye.

**41.** Simu ndogo ambayo mtu anaweza akatembea nayo mahali popote inaitwa
A. simu tamba
B. simu ya nyumbani
C. simu ya *ofisi*
D. arafa

**42.** Rununu ni kifaa cha ya kisasa.
A. maliasili
B. ajira
C. teknolojia
D. madini

43. Rununu pia haiitwi
A. ofisi
B. selula
C. rukono
D. simu tamba

44. Kadi ambayo hununuliwa yenye nambari fulani za rununu ambazo mtu hutumia kwa kitambulisho chake pekee huitwa
A. ajira
B. kadi
C. simu kadi
D. simu hela

45. Ipi si manufaa ya rununu?
A. Kutuma arafa.
B. Kuwapa watu ajira.
C. Kuwaibia watu pesa.
D. Kupata pesa kwa kutengeneza rununu zilizoharibika.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

46. Manufaa ya rununu ni **tumbi** tumbi.
Maana ya tumbi tumbi ni
A. si tele
B. chache
C. nyingi
D. haba

47. Maana ya neno "**ajira**" ni
A. kazi
B. pesa
C. malipo
D. ela

**48.** Ni methali gani inalingana na maelezo haya: Rununu, hata kama ni kifaa kidogo, kina faida nyingi?
A. Enga kabla ya kujenga.
B. Hakuna kizuri kisichokuwa na ila.
C. Majuto ni mjukuu huja kinyume.
D. Usione wembamba wa reli gari moshi hupita.

**49.** Mojawapo ya hasara za rununu ni
A. kuuza rununu na vifaa vyake kwa malipo kwenye duka la simu kama mfanyi kazi.
B. kuwasiliana na marafiki.
C. kutuma ujumbe wa chuki na matusi.
D. kuajiriwa katika duka la M-pesa.

**50.** Kichwa mwafaka cha kifungu hiki ni
A. Kadihela
B. Rununu
C. Mawasiliano
D. Arafa

&Stepford Press and Publishers, 2021